TANGAZO LA SERIKALI NA. 875 la tarehe 1/12/2023

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA MAJI KWA AJILI YA USIMAMIZI WA MIRADI YA MAJI KATIKA MIJI YA KAYANGA, CHATO NA GEITA YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa gari moja linaloingizwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya Usimamizi wa Mradi wa Maji katika Miji ya Kayanga, Chato na Geita ya Mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 3 Novemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari moja lililoainishwa kwenye Jedwali, linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Maji umesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika Ukomo tarehe 02 Mei, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chesisi | Idadi | Mahali |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Landcruiser 4wd Station Wagon | JTMAACBJ304027808 | 1 | Imeingizwa nchini |

Dodoma,
21 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*